Jiwe la kiroho la kujengea na. 155

## KUTIA NANGA NDANI YA KRISTO NENO

*Waebrania 6:18-20 "…….Sisi tuliokimbilia kuyashika matumaini yale yawe kwayo mbele yetu tuliyonayo kama nanga ya roho, yenye salama, yenye nguvu, yaingiayo hata mle mlimo ndani ya pazia, alimoingia Yesu kwa ajili yetu, mtangulizi wetu, amekuwa kuhani mkuu hata milele kwa mfano wa Melkizedeki".*

Mhuduma mmoja mzuri alisema muda mfupi ulipita, alisema, "Ndugu Branham, kama tu ningeweza kuwa na furaha ya Bwana ndani ya moyo wangu …….."

Nikamwambia, "Mwanangu, uamsho umeisha". Unaona? Sasa, vitu vya kuondoa kuyumba yumba vimeshawekwa kwenye meli. Mawimbi makubwa ya kutisha yako mbele yetu, lakini tunajua mbele ya hayo mawimbi kule tunakaribia pwani. Unaona? Kaa usiyumbe yumbe. Kaa katika Neno; kaa na Mungu. Haijalishi unajisikiaje, wala kitu chochote, kaa na ushikilie Neno sawasawa. Iache isiyumbe yumbe. Wakati unapoona mawingu haya makubwa yakituzunguka, na dhoruba zinakuja, na mabomu ya atomiki, na vitu vinginevyo wanavyovizungumzia; lakini kitu kinachotushikilia tusiyumbe ni hasa moja kwa moja ni Neno. Mungu alisema litakuwa hapa; tutayapanda/kuyavuka kila moja. Ndiyo vema tutaenda juu ya kila moja. Ndiyo, hakika. Hayawezi kutuzamisha; hayawezi kutuua sisi. Ukituweka kaburini; tutakuja kufufuka tena. Na hilo ndilo lililopo. Hakuna njia duniani ya kuliweka chini pale tutavuka kila wimbi, kwa sababu kapteni wetu mkuu anaita ule upande wa pili.

Iwavyo vyote, naije, ijayo, jinsi itakavyo, haifanyi tofauti; tumeweka nanga hasa ndani ya Yesu; kama ninaishi; nitaishi kwa utukufu wa Mungu kama ninakufa, nitakufa kwa utukufu wa Mungu. Kile tu ambacho ni kwa utukufu wa Mungu ndicho nitakacho kifanya. Yote yakiisha, sitaki kukaa na kungoja tena. Nataka niende kupokea thawabu yangu ambayo ameninunulia, sio ile niliyopata mimi, lakini ni ile aliyoninunulia mimi, kile alichonipa mimi kwa Neema yake. (Ufunuo 22:12) [1]

Na Mkristo aliyezaliwa mara ya pili amefungwa na Kristo, na Biblia ndiyo Nanga (1Petro 1:23). Ni kile kitu tulichofungiwa kwake. Acha madhehebu, acha vitu tofauti, acha sayansi, acha waelimishaji waseme chochote watakacho kusema. Ili mradi Neno linasema hivyo na imeahidiwa hivyo, tumefungiwa kwa hilo. Kuna kitu fulani hakingeturuhusu tusogezwe kutoka hilo. Hiyo ni kweli. Mkristo halisi aliyezaliwa mara ya pili, anashikilia lile Neno. Kama Linasema fanya jambo fulani, hiyo ndiyo namna ya kulifanya. Haijalishi vile mtu mwingine atasema, hivyo ndivyo



Mungu alivyosema. Tumefungiwa na hilo, maisha ambayo chimbuko lake ni kwa Kristo.
Hiyo ni nanga kwa meli. Meli imefungwa kwenye nanga wakati wa dhoruba. Na kama Kristo ni yakini yako, umefungiwa kwake. Wakati wa taabu, meli kama utaiachia iyumbe, itavunjika kwenye hayo mawe, lakini wanachofanya, wanashusha nanga. Ile nanga inajichimbia mpaka inajikita kwenye msingi wa mawe. Na meli imefungiwa kwenye nanga. Ni yakini ya hiyo meli [2].

Sasa, kama watu wagonjwa ambao wako katika jengo, watu viwete au wewe ambaye unauhitaji na Mungu, kama utapata aina hiyo ya ufunuo kwamba umehesabiwa haki (1kor.6:11) unapojua hakika kwamba umehesabiwa haki kwa kuomba kitu kile unachokiomba, na kwamba Yeye anawapa thawabu wale wanaomuomba/wanaomtafuta Yeye (Waebrania 11:6), Hakuna kinachoweza kututenganisha na imani hiyo iliyotia Nanga ndani yako (Rumi 8:38-39). Unaona? Lakini kwanza lazima ifunuliwe kwako. [3].

Na Ibrahimu aliacha nchi, akawa mkimbizi, akajiita mwenyewe ni mgeni na msafiri (Waebrania 11:8-10). Na angalia, Ibrahimu kama wanadamu wote ni wa muda, sio watu wasiokufa, sio mtu ambaye hafanyi makosa, lakini alifanya makosa kila mara (Mwanzo 12:10-20; 20:1-18). Lakini haijalishi ni makosa mangapi yeye aliyafanya Nanga yake bado ilishikilia, kwa maana alikuwa na ahadi [4].

Lakini ninakuambia, mtu halisi mwanaume au mwanamke ambaye amezaliwa na Roho wa Mungu atakaa sasa baada ya saa akinywa kutoka kwenye Neno la Mungu. Siyo hiyo tu, lakini linapogonga/kumfikia pale, linatia Nanga, na kubadilisha maisha. [5].

Utaondoka ukienda zako ukiwa mtu tofauti utaenda zako ukiwa na Nanga ndani ya nafsi, kwamba hukuna kinachoweza kukuondoa pale unajua kwamba umeponywa.

Unajua kwamba Mungu amelishughulikia hilo jambo kwa ajili yako, kwa sababu Yeye ameahidi [6]

Mungu hukuwekea Nanga ya kitu fulani kidogo ndani ya moyo wako na kusema, "Hiki ndicho" "Kiamini hicho". Shikilia hicho. Hilo ni Neno la Mungu. Ameahidi naye atalithibitisha kwako. Na kama Anathibitisha Neno, lishikilie hilo [7].

Nimeshikilia kwenye Nanga hiyo kule katika Mwamba. Mawimbi yananiyumbisha mimi juu na chini kuzunguka, lakini Nanga yangu imeshikilia. Iko ndani ya Kristo na Neno lake. Ninaamini Neno lako ni kweli. [8].

"Matumaini tuliyo nayo kama nanga ya roho, yenye salama, na yenye nguvu ………." (waebrania 6:19).

Siyo kuyumbishwa na kila fundisho na kila upepo, ukiyumbishwa kutoka upande huu hata ule, ukichukua upande hapa, na kuchukua upande pale, hujui

unaposimamia. Biblia ilisema, “Ningetaka muwe imara”, siyo kusema, “vema, leo niko hivi na kesho kitu kingine”. Itilie nafsi yako nanga ndani ya Yesu Kristo. Zaliwa mara ya pili, maisha ya Mungu yakiishi ndan yako, na unajua bila shaka yoyote, kwamba umepita kutoka mautini na kuingia uzimani. (Yohana 5:24). Tumaini lako lote limejengwa kule msalabani. Upendo wa Mungu unamwagikia kupitia moyo wako. Na unaamini kila Neno ambalo Mungu amesema ni kweli uko tayari kufa kwa kifungu chochote cha hilo. Unaona ninacho maanisha? Yenye kushikilia na yenye uhakika [9].

Kama unataka kujiwekea nanga mwenyewe, weka nanga ya hilo Neno moyoni mwako. Daudi alisema ameliweka ndani ya moyo wake asije akatenda dhambi (Zaburi 119:11). Ameziandika sheria zake katika nguzo za kitanda na akazifunga kwa mikono yake na kila mahali, ameliweka Neno lake mbele zake (Zaburi 16:8, Kumbukumbu ya Torati 6:4-9). Hiyo ndiyo njia. Weka mawazo yako wakati wote …..[10]

Acha mawimbi yavume; nanga yangu imeshikilia mafichoni. Siwezi kukueleza kwa nini siku hizi tuna mawimbi mengi katika bahari, lakini ninashukuru kwa ajili ya nanga inayoshikilia kwa nguvu mafichoni. Wakati inayumba yumba na inaonekana kana kwamba kila hatua itaipeleka chini, bado nanga yangu iko mafichoni, nimeweka nanga mafichoni. [11].

Kama kijana mdogo aliyerusha tiara aliulizwa, iko wapi? Alisema, sijui, lakini iko kule mbali mahali fulani; naweza kuisikia mwishoni mwa kamba. “Hilo hapo”.

Mwanaume au mwanamke ambaye analichukua Neno la Mungu, ameshikilia kitu fulani. Nanga yako imeshikilia mafichoni. Mawimbi na dhoruba vinaweza vikasonga na kutingisha katika kila njia. Lakini umewekewa nanga. Inakuja pale pale mahali pake. Unang’ang’ania. Unaenda kuamini hivyo.

Nuhu aliliamini hivyo, hakika, na alitimiza lengo la Mungu kaitka maisha yake. Unapenda kutimiza lengo la Mungu kaitka maisha yako? Hivyo kuwa unayeng’ang’ania unapolipata Neno. Lishikilie, ile ahadi; ni yako. [12].

Usiitenganishe nanga yako na kalvari. Shikilia sana Neno la Mungu, kwa maana “Juu ya mwamba huu nitalijenga kanisa langu” kaa na hilo (Matayo 16:13-18). [13]

Na kama umetia nanga yako katika Neno, na Neno limetiwa nanga kwako, wewe ni wa milele pamoja na Neno. Amina lazima lije kwenye mwisho wake. Mambo haya yote yanatetemeshwa haijalishi wanajenga nguzo kiasi gani, lazima itaanguka chini. Vitu vyote ambavyo sio vya au kinyume na Neno au vinapishana nalo, vitaondoka. Lazima vitoe nafasi, kwa sababu Neno linakuja kwenye ushindi. Hakuna kiwezacho kulizuia. Mungu amekwisha kusema hivyo. Anapolinena, mbingu na nchi zitapita, lakini Neno kamwe halitashindwa (Matayo 24:35) Lifiche hilo Neno moyoni mwako. Namna ya kulichukua hilo Neno kuliachilia likue … Liweke akilini mwako siku zote (2Tim.2:8), kwa sababu kamwe haliwezi kushindwa. Neno la Mungu



kamwe halishindwi, kwa sababu amesema haliwezi kushindwa. Kwa hiyo tunataka kulishikilia hivyo. [10].

Oh ndugu yangu, dada; sasa, kila mtu awe na ufahamu kwani najua hiyo inamaanisha nini, unaona? Angalieni tu, kaeni karibu na Kristo. Hebu niwaonye ninyi sasa, kama mhudumu wa injili kwamba hii … Msichukue upuuzi wowote, msijairbu kuwazia chochote. Kaeni pale mpaka ule utu wa ndani umeweka nanga katika Neno, kwamba kwa hakika uko ndani ya Kristo. Kwa sababu hicho ndicho kitu pekee kitakacho …… kwa sababu tuko katika wakati wa udanganyiuf sana ambao tumewahi kuishi ndani yake. Utamdanganya hata aliye mteule kama itawezekana Matayo 24:24 kwa sababu wanao upako. Wanaweza wakafanya vyovyote kama na hao wengineo wote.

Safisheni maisha yenu; lipeni madeni yenu; usidaiwe na mtu chochote. Yesu alisema, “Sasa ……. Sasa, simaanishi kitu kama kodi ya nyumba au vitu kama hivyo. Lazima tufanye hivyo. Yaweke mambo yako yote sawa. Hakikisha kila kitu kiko sawa kuwa tayari. Jiandae, kumbukeni nasema haya katika Jina la Bwana, jambo fulani litaenda kutokea [14}

Nimekusudia kufanya kila niwezacho kuwashawishi wanaume na wanawake – tafadhali kueni na uhakika na hili! kama upendo wa Mungu haukuweka nanga imara moyoni mwako usichukue msisimko au kujisikia. Hakikisha unaweza kugeuza shavu lako upande wa pili, kwamba kwako kristo ni yote katika yote usikose hilo ndugu yangu. [15]

<u>**Nukuu za Kiingereza**</u>

[1] Kristo akifunuliwa katika Neno lake Aya 155 – 157
[2] Yakini (63 – 1201M), Aya 66 – 68
[3] Nimesikia lakini sasa ninaona Aya 57
[4] Melkizedeki Yule mfalme mkuu ajaye Aya 48
[5] Njia ya Nabii wa kweli Aya 92
[6] Mungu ana njia aliyotupa (56-0108) Aya 22
[7] Mungu asiyebadilika (60 –0326) Aya 16
[8] Kuhukumiwa kwa uwakilishi (60 – 111), uk 35
[9] Aliapa kwa nafsi yake Aya 230[10] sauti zisizo na uhakika (63 – 0114) Aya 35 – 37
[11] Kwa nini watu wanayumbishwa huku na huku (56 – 0101), uk 27
[12] Kung’ang’ania Aya 105 – 108 [13] Mjumbe wa jioni Aya 193
[14] Nawe hujui uk. 36 – 37 [15] Tangu wakati huo (60 – 0716, Aya 106

Jiwe la kiroho la kujengea na. I55 kutoka kwenye Neno lililofunuliwa la saa hii yamekusanywa na Gerd Rodewald friedenstr.69, D-75328 Schonberg, Germany simu (+49) 2357613 Fax (+49) 72363306

Anakuja mmoja na ujumbe ambao ni moja kwa moja ni Biblia na kazi ya haraka itazunguka dunia. Na mbegu zitaingia magazetini, vitu vya kusomea, mpaka kla mbegu iliyokusudiwa kiumbe imesikia (Ndugu Braham katika mwendo utaratibu na mafundihso uk. 724) .

Kwa nakala zaidi kiingereza kiswahili andika kwa:
Charles E. Y. Kanju,
Box 5138, Tanga